SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA WAATHIRIKA
WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU 2023

TUME YA KIMATAIFA YA HAKI ZA BINADAMU

JESHI LA WOKOVU

# NIMESIKIA VILIO VYAO



## MWONGOZO WA MAOMBI DUNIANI

### MAOMBI KWA WAATHIRIKA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

wale ambao bado wamenaswa

Mungu wa haki, tumaini,
na Mungu wa upendo kwa wasio na baba,
mtetezi wa wanaokandamizwa, tumaini letu kwa miaka ijayo.
Tunaamini kwamba ni kwa ajili ya uhuru umetuweka huru,
tutumikiane katika upendo ili tuishi katika wingi na wema.

Mpendwa Mungu,
Katika wakati huu,
tunasimama pamoja na dada na kaka zetu,
wanaume na wanawake,
wavulana na  wasichana hata pamoja na yote
wanayofanya ambayo inawezekana hatuyajui.

Bwana, twaomba uwakomboe kutokana
na mikono ya wanao wakandamiza,
watoe katika kibano cha waovu na kwa neema
yako rejesha maisha yao na uwalete kwenye mwanga.
Wasaidie wapone, wajalie wapate haki na twaomba
waliowasafirisha watubu na wafikie kukufahamu wewe zaidi.

Tujaze na huruma yako takatifu na upendo ili
tuweze kuendelea kupambana kupata haki.
Tutumie kama chombo chako, kusaidia
kukomesha mateso haya ya binadamu.
Na twaomba upendo wako, ukumbatie na
uwepo wako usiondoke kwa waathirika hawa.
Sikia kilio na maombi yetu ewe Baba wa Mbinguni.

Amina!

**Joy Ime-Sunday,** *Teritori ya Nigeria*

---

## MAOMBI KWA AJILI YA WANUSURIKA… NA WANUSURIKA

wale waliowekwa huru kutokana na usafirishaji haramu

*Malaika Oringo, Mtaalamu Duniani wa Ushiriki wa Walionusurika na ujumuishaji anachangia: 'Kwa wanusurika wote waliopotea baada ya utumwa, msipoteze tumaini; Yesu ni mwaminifu kwa ahadi zake. Alisikia kilio changu kama mnusurika, na kwa sababu ya hili, tafadhali fahamu hauko peke yako. Haya ndiyo maombi yetu kwako.'*

Tunasikia vilio vyao! Wanusurika wa usafirishaji haramu wa binadamu wameungana katika maombi kwa ajili ya wanusurika wengine. Tunaomba kwa ajili ya tumaini na kurejeshwa. Tunasikia kwa masikio na kwa mwili vilio vya wanusurika; tunaelewa ni wangapi ambao wamevumilia mshituko mkubwa hata baada ya utumwa.

Bwana, sikia vilio vyao vya kuhitaji amani ya ndani; tunakuja mbele zako kama watu waliovunjika moyo. Tunalilia uponyaji kwa ajili ya wanusurika wengine wanaoshughulika na vidonda ambavyo vimeenea sana na haviwezi kupona vyenyewe. Waponye wanusurika watokane na maumivu ya kumbukumbu za mambo ya nyuma.

Mungu mwaminifu na mwenye huruma, sikia vilio vyao katika maombi ili kurejesha uwezo wa kuamini wa hizi nafsi zilizojeruhiwa waamini kwamba watu wanaweza kuwa wema, wenye upendo, na wapole. Twaomba urejeshe mahusiano yanayoweza kusaidia wanusurika waungane na marafiki na familia zao, badala ya wasiwasi na huzuni wapewe tumaini na kuona wanusurika wanastahili.

**Malaika Oringo,** *Teritori ya Uholanzi, Jamhuri ya Czech na Slovakia*

---

'Kwa wanusurika wote waliopotea baada ya utumwa, **msipoteze tumaini** ; Yesu ni mwaminifu kwa ahadi zake'

## MAOMBI YA HAKI YA KUREJESHWA

**Mpendwa Mungu wa Haki:** Tunasikia vilio vya watu walionaswa katika matukio ya utumwa wa kileo na unyanyasaji.

Tunazidiwa, tunashangazwa na tunahaja ya haki kwa ajili ya wale wasio na uwezo wa kujilinda, wanaonyonywa na waliosahaulika.

Mungu wa mwangaza, tunaomba haki yako ya haraka kwa ajili ya wale wote walionaswa katika utumwa wa kileo na unyonyaji.

Tunahitaji haki. Tunaomba kwa ajili ya upatanisho kwa ajili ya makosa yaliyofanywa na wahalifu na twaomba uichome mioyo yao kwa mwanga wako wa haki na uwasaidie kwa unyenyekevu watubu na wageuke kutoka katika njia zao ovu.

Tunaomba kwamba wahalifu wageukie jukumu la kusaidia kuzuia wengine kujishughulisha na uonevu wa wanadamu.

Ndivyo tunavyoomba, amina!

**Emmanuel Wataka,** *Teritori ya Uganda*

---

## MAOMBI KWA AJILI YA KANISA DUNIANI

Mpendwa Bwana, Mungu Mkuu, Mungu wa uhuru:

Kuna watu wengi sana kutuzunguka wasioonekana wala hawasikiki katika mazingira yao tatanishi.

'Tangu nilipo kamilisha miaka 13, kila siku nalazimishwa ukahaba na kubakwa…siwezi kuendelea nayo kamwe…nani anaweza kunisaidia?'

**Tunasikia kilio chako!**

'Nilipelekwa ng'ambo na wazazi wangu kutafuta fedha, lakini hawa watu hawanilipi na wananitendea vibaya. Nafanya kazi kwa bidii masaa 16 kwa siku. Siwezi kuendelea zaidi ya hapa… nani anaweza kunisaidia?'

**Tunasikia kilio chako!**

'Nimemtoroka mume wangu na nimetoroka ukatili wa nyumbani. Sasa najaribu kutafuta aina yoyote ya kazi ili niweze kuwatunza watoto wangu…lakini kazi ambayo bwana huyu ananipa inaonekana sio kazi salama. Sina fedha, naogopa, sijui nifanye nini…nani anaweza kunisaidia?'

**Tunasikia kilio chako!**

Ewe Bwana, unadai haki kwa ajili ya watoto wako waliofanyiwa makosa.

Tusaidie sisi kama kanisa duniani tufanye kazi pamoja tusikie kilio chao kama wewe. Fungua macho yetu, tusaidie tuwe imara, tusimame na kupigana kwa ajili ya wale ambao wanaogopa, hawana nguvu na hawana sauti. Haya ni mapambano yako, ushindi wako, utukufu wako!

Katika jina la Yesu, amina!

**Galina Ketroy,** *Teritori ya Ulaya Mashariki*

---

## MAOMBI KWA AJILI YA JITIHADA ZA JESHI LA WOKOVU DUNIANI ZA UTUMWA WA KILEO NA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

Mungu Baba, kama pamoja na Waisraeli miaka maelfu iliyopita, tunaomba kwa ujasiri kwa muda huu tukitambua utasikia vilio vyetu, hasa kwa ajili ya haki kwa wale waliokosewa kwa unyonyaji wa ngono na kazi za kulazimishwa.

Kwa waliokandamizwa na wapungukiwa wanaopitia giza, tunaomba kwamba uangaze mwanga wa matumaini na amani. Tafadhali vunja minyororo ya wale wanaowafunga wengine katika utumwa na umaskini na kwamba watoto wote wa Mungu wapate baraka ya uhuru na nafasi ya kuishi maisha ya thamani na yenye afya.

Bwana, twaomba uwape ujasiri wale watu jasiri wanaofanya kazi na waathirika na wanusurika wa unyonyaji wa ngono na kazi za kulazimishwa. Wahimize katika roho zao, mioyo na miili yao, na uwape wafanyakazi hawa rasilimali wanazohitaji ili kuwasaidia wale waliokumbwa na ukosefu wa haki duniani.

Tunakushukuru Bwana, kwamba wewe ni Mungu unayetusikia sisi, El Roi. Twaomba mioyo yetu iungane pamoja tunapopaza sauti zetu tukiomba kwa ajili ya uhuru na haki kwa wote.

Bwana, asante kwa kusikia vilio vyetu.

Amina!

**Kamishena Shelley Hill,** *Kanda ya Marekani na Caribbean*

## MAOMBI YA KUJITOA YA ALLY

Nasikia vilio vya watoto wa kike na wa kiume kupita giza lililotanda, waliosafirishwa na kuwekwa utumwani kwa manufaa ya wengine.

**Nasimama nanyi.**

Naona kizazi kifuatacho cha watoto katika mazingira hatarishi wanaolengwa kwa manufaa ya furaha za kidunia.

**Nitapigana kwa ajili yenu.**

Nasimama na watendaji walio mstari wa mbele, wanaotetea uhuru wa waathirika wa ukandamizaji na natembea pamoja na wanusurika.

**Nawatambua ninyi.**

Naomboleza kwa jinsi nimechangia kwa kufahamu na kwa kutokufahamu utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu kupitia kwa ujinga wangu, nafasi yangu na nguvu yangu ya matumizi.

**Nakataa kuwa kipofu.**

Naomba maombi yangu na yale ya watu wako yageuke kuwa tendo tunapopambana pamoja dhidi ya ukosefu wa haki.

**Hatuko huru mpaka sote tuuone mwanga.**

**Jean Nangwala,** *Teritori ya Zambia*

---

'Naomba maombi yangu na yale ya watu wako yageuke kuwa tendo **tunapopambana pamoja dhidi ya ukosefu wa haki**'